

TANGAZO

HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA – MTWARA



TAREHE 03/04/2018

NAFASI YA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mbadala kwa watendaji wa vijiji na mitaa chenye Kumb.CFC.26/205/01"FF"/99 cha tarehe 22 Agosti,2017 kikisomwa kwa pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha ajira mbadala kwa watendaji wa vijiji na mitaa yenye Kumb Na.CFC26/205/01"GG"/95 ya tarehe 12Machi,2018. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba anapenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

A. WATENDAJI WA VIJIKI – NAFASI 98

(i)Kazi na majukumu

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao,kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mpango ya maendeleo ya kijiji
- Katibu wa mikutano ya Kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na Taratibu
- Kuandaa taarifa z utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji

- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
- Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na mwajiri

(ii) SIFA NA UZOEFU

- Awe na Elimu ya kidato cha nne(IV) au sita(VI)
- Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika fani zifuatazo:-
Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinacho tambuliwa na Serikali

(iii) MSHAHARA

Ngazi ya mshahara itakuwa TGS B1- 390,000/= kwa mwezi

B.MAELEZO/MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi miaka 45.
2. Barua iambatanishwe na wasifu binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni(Curriculum Vitae) anuani inayotumika, namba ya simu na anuani ya barua pepe(e-mail address).
3. Barua ya maombi iambatanishwe na vivuli vya vyeti vilivyothibitishwa ambavyo ni
 - a) Vivuli vya Cheti cha kidato cha nne
 - b) Kivuli cha cheti cha NTA 5 kwa vyuo vilivyopo chini ya NACTE
 - c) Kivuli cha Cheti cha kuzaliwa
4. Waombaji wawe wenye zile sifa na uzoefu uliotajwa kwenye tangazo hili la kazi.
5. Picha 2 ndogo(passport size) za hivi karibuni.


6. Matokeo ya muda(provisional/testimonials/statement of results) havitakubaliwa
7. Waajariwa wa serikali maombi ya barua yapitie kwa mwajiri wake
8. Waombaji wataoleta maombi na vyeti vya kughushi hatua za kisheria zitachukuliwa
9. Waombaji wa makundi maalum wanashawishiwa kuomba.
10. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na sita vya nje ya nchi vifanyiwe ulinganishi na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.
11. Waombaji wenye vyeti vya astashahada na diploma vya nje ya nchi vifanyiwe ulinganishi na NACTE na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi .
12. Waombaji kwenye wasifu binafsi(CV) watatakiwa kuweka wadhamini(referees) watatu wanaofahamika.
13. Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza
14. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni Ijumaa, tarehe 16/04/2018 saa 9.30 alasiri

Barua zote zitumwe kwa
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba,
S.L.P 03,
Tandahimba.

Nakala: Mbao za Matangazo

Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba:- www.tandahimba.go.tz

IMETOLEWA



SAID. A. MSOMOKA
MKURUGENZI MTENDAJI(W)
TANDAHIMBA

MKURUGENZI MTENDAJI(W)
S.L.P 03
TANDAHIMBA